Mwishowe, nawaomba Wakenya wote kukumbuka kwamba, matokeo ya siku zijazo ya Taifa la Kenya ni lazima yatayarishwe na wananchi wa Kenya wenyewe. Na lazima iwe ni lengo la kila mmoja wetu kuhakikisha kwamba wananchi wa Kenya wameungana pamoja; na kwamba wanapendana na wanaishi pamoja kwa amani. Hii ina maana kwamba sisi sote ni lazima tuongozwe na falsafa ya Nyayo ya Amani, Upendo na Umoja.

*HARAMBEE!!! NYAYO!!!*



*Rais.*

# MANIFESTO YA KANU

## 1. Asili na Maumbile ya KANU

1.1. *Kuendelea Daima.*—Maumbile ya KANU yanaweza kueleweka na kutambulikana katika mazingira ya Kenya. Kwani asili na kuendelea kwa umbo lake ni sehemu muhimu ya historia ya Kenya. Chama hiki kilizaliwa kutokana na hamu na tamaa kubwa ya kutaka uhuru wa wananchi wa Kenya, na moyo huu ndio ukawa ni sababu kubwa ya kuzaliwa kwa KANU, na ni moyo huu ndio ambao unadumisha KANU, moyo ambao unapatikana katika falsafa tukufu ya ujamaa wa Kiafrika. Maumbile na kazi kubwa inayofanywa na KANU inaendelea daima kutokana na hamu na matakwa ya nyakati zinazobadilika-badilika. Hata hivyo, KANU ni chama cha kisiasa na chombo cha harakati cha wananchi kinachojitolea kutetea uhuru wa Kenya na mamlaka kamili ya kitaifa, wakati ambapo amani na umoja unaleta kwa urahisi maendeleo katika nyanja zote.

1.2. *Chama.*—Kutokana na mahitaji makubwa ya kitaifa ili yalete mfumo wa Kiafrika wa usimamizi wa kijamii na kisiasa kwa manufaa ya jamii na umma, wananchi wa Kenya walichagua kwa hiari yao wenyewe demokrasia ya kuwa na chama kimoja, na kwa njia hii KANU inalindwa ndani ya katiba ya taifa. Kama Chama, KANU inayo wajibu wa kisiasa wa kuliongoza taifa na kuunda Serikali thabiti kwa ajili ya kuendeleza masilahi ya Wakenya.

1.3. *KANU kama Chombo cha Harakati kwa Wananchi.*—Katika umbo lake jingine KANU ni lazima kibaki na kuwa chombo muhimu cha kuwaunganisha watu tofauti tofauti na jamii mbali mbali wa Kenya na kuwa taifa lenye umoja, lenye umbo la fahari, taifa lenye kuthamini asili na utamaduni wake. KANU siku zote itaendelea kufanya juhudi ya kuyaleta mambo haya.

## 2. Msingi Imara: Malengo, Shabaha na Shughuli za KANU

Lengo halisi na shughuli za KANU inabaki ile ile ya kudumisha taifa huru la Kenya, kuendeleza masilahi ya Wakenya, pamoja na kudumisha amani na ustaarabu wa mwanadamu.

2.1. *Maelezo ya Kimsingi ya Ujamaa wa Kiafrika.*—Hazina ya asili iliyoleta falsafa ya Nyayo na harakati za harambee ni ujamaa wa Kiafrika. Na kutokana na haya tunapata muundo wa Kiafrika wa maadili, wenye kukusanya pamoja ari ya kujitegemea na kuungana mkono kwa pamoja katika jamii. Haya ni maadili ya asili na misingi itakayoendelea kuongoza siasa za KANU na mipango yake siku zijazo.

2.2. Kutokana na maadili haya ya asili ni miongozo ya ujenzi wa taifa na marekebisho mema ya kijamii na kiuchumi. Kwa hivyo, KANU imekusudia kuyaunganisha pamoja makabila mbali mbali na watu wote wa Kenya katika taifa moja lenye umoja kwa kuondoa vikwazo vyote vya kikabila na vya kitamaduni. Na wakati wa kuunda taifa, KANU inajitahidi kuvilinda vyombo vyenye thamani na maadili ya Kiafrika kwa kuendeleza siasa ya utulivu ya kijamii na kitamaduni. KANU inaamini kufanya marekebisho yanapohitajika, pamoja na kufanya mipango na usimamizi wa mfumo wa kisiasa unaombatana na tamaduni za Kiafrika na shughuli zake. Kwa hivyo, KANU imefuata njia ya kuwashirikisha wananchi wote kwa jumla katika kazi ya kuwateua wagombea uteuzi wa Chama kwenye uchaguzi ujao wa bunge na uchaguzi wa serikali za mitaa. Kwa kufuatana na misingi hii, KANU itaendelea siku zote kuwashirikisha wananchi katika kutoa uamuzi wao na kwenye matayarisho ya miradi ya maendeleo, na pia katika kuchukua pamoja majukumu ya fedha pamoja na majukumu mengine kwa ajili ya kuleta usitawi katika jamii na Serikali. Kwa kufuata njia hii, KANU inafanya juhudi ya kuziunganisha bidii za wananchi, pamoja na kuzishirikisha miradi yote ya harambee kwenye Mipango ya Maendeleo ya Wilaya inayoongozwa na Kamati za Maendeleo ya Wilaya. KANU halikadhalika inajitahidi kurekebisha na kusitawisha masilahi ya Wakenya wote.

2.3. Kwa kutokana na hayo yalioletajwa hapo juu, KANU inathibitisha upya kwamba maendeleo ya kudumu yanaweza tu kupatikana iwapo kutakuwa na amani inayoletwa na umoja wa kitaifa ili kuimarisha utulivu. Na ili yapatikane mambo haya KANU itafanya juhudi ya:

- (i) Kulinda haki za kimsingi za kibinadamu, uhuru na haki zake zote, kama vile haki ya kuishi, ya kumiliki mali, na uhuru wa kujumuika na watu wengine, pamoja na uhuru wa kutamka.

- (ii) Kuhimiza kuvumbua upya na matumizi ya maadili ya Kiafrika na mfumo wake, kuunganisha shughuli za kijamii na kitamaduni kwa lengo la kuleta usitawi, na kujithamini sisi wenyewe pamoja kuthamini asili zetu.
- (iii) Kuhimiza kazi ya ujenzi wa taifa, pamoja na kulinda uhuru wa Taifa la Kenya.
- (iv) Kuongoza barabara pamoja kulitawala taifa, huku kunaendelezwa masilahi ya Wakenya, kwa njia ya kutayarisha na kufanya mipangc itakayoleta uzalishaji wa kiwango cha juu.

2.4. Na hatimaye, KANU inatilia mkazo umuhimu wa nidhamu katika kuimarisha mfumo wa manufaa na kukua kitaifa—nidhamu ya binafsi, nidhamu ya jamii, nidhamu ya Chama na nidhamu ya kitaifa. Kwa njia hii, wananchi si kuwa watapata hisa zao halisi zinazotokana na maendeleo, lakini hata katika juhudi zao za kuzalisha mali zinazoleta manufaa haya. KANU, pamoja na hayo, inaamini katika kuunganisha juhudi zote zinazotokana na Chama, wananchi, Serikali na kutokana na kuelewa kikamilifu falsafa ya Nyayo pamoja na harakati za harambee.

### **3. Uhifadhi wa Mazingira**

3.1. Shughuli muhimu ya KANU katika uwanja wa mazingira katika hatua ya sasa ya maendeleo ya Kenya ni kuhakikisha kwamba kunapatikana uzani kati ya shughuli za binadamu na uhifadhi wa kimazingira.

3.2. Serikali ya KANU kwa hivyo imeanzisha mpango wa muda mrefu wa kusimamia ardhi kwa kufuata shughuli za uzalishaji katika kanda za kimazingira, na wakati huo huo kufanya majaribio mapya ili kupatikane maendeleo ya maliasili.

3.3. Upandaji upya wa miti ni sehemu ya mipango mikubwa kwenye uhifadhi wa ardhi. Jambo hili linatokana na utambuzi wa kwamba misitu inaathiri hali ya hewa, uzalishaji unaotokana na ardhi, na inalinda maeneo ya kupatikana kwa maji.

3.4. Serikali ya KANU itapanua juhudi zake za kupanda miti upya kwa kuchukua hatua zinazofaa na kwa njia za kuwaelimisha wananchi. Kwa njia hizi upandaji miti hasa ile miti ya kiasili uitamarishwa. Na ili kurahisisha jambo hili, nasari za miche

zimekwisha anzishwa kote nchini. Elimu ya kimazingira inatolewa kwenye shule na kwenginepo. Na hatari ya kuharibu mazingira na kwa upande mwingine hatua za uhifadhi wa kimazingira yote haya, yatakua ni sehemu muhimu ya elimu ya kimazingira.

3.5. Sera ya Serikali ya KANU kuhusika na misitu pia ina lengo la kuhimiza kupatikana kwa kazi na kuongeza kupatikana nchini kwa wingi mbao na mazao mengine ya misitu. Serikali ya KANU inatambua kwamba misitu ina thamani kubwa, si kwa ajili ya sababu za kiuchumi na za kimazingira, lakini ni kwa sababu maeneo ya misitu yana uzuri wa mandari ya kimaumbile.

3.6. Serikali ya KANU imeweka rasilimali kubwa kwenye mpango wa kisasa wa kuelewa hali ya hewa na kupatikana kwa maji, mpango ambao utakuwa ukitowa maelezo kamili juu ya kupatikana kwa uhakika maliasili ya maji ya nchi, na kutoa tathmini juu ya uwezekano nchini wa mipango ya kumwagilia maji na mipango ya kupatikana kwa nishati kwa nguvu za maji.

3.7. Serikali ya KANU imekwisha anzisha vyuo kadha wa kadha juu ya shughuli maalum za kimazingira. Hivi ni:

- (i) Wizara ya Mazingira na Maliasili
- (ii) Tume ya Rais ya Kudumu ya Upandaji Miti, Maji na Uhifadhi wa Udongo.
- (iii) Shule ya Masomo ya Mazingira.

3.8. Pamoja na hayo yaliyotajwa juu, mamlaka ya ustawi zimekwisha anzishwa kusimamia mipango ya maendeleo kwenye mabonde ya mito. Serikali ya KANU pamoja na haya yote inahimiza mashirika yasiyokuwa ya Serikali ili yajishughulisha kwenye uhifadhi wa mazingira.

3.9. Shabaha ya jumla ya KANU kwa ajili ya usitawi wa maliasili ya madini ni kutafuta manufaa makubwa kabisa kwa ajili ya nchi kwa kuyapata kwa kutumia utafiti maliasili hizi zisizoweza kupatikana tena upya. Kugunduliwa na hatimaye kupatikana kwa madini unatarajiwa kupatikana kwa kazi, mapato ya fedha za kigeni na kutoa mchango kwa mpango kwa muda mrefu kwa ajili ya kupatikana kwa maendeleo ya viwanda.

3.10. Serikali ya KANU itaimarisha vyombo vinavyohitajika kwa ajili ya kutathmini na kusimamia mabadiliko ya kimazingira

yanayoweza kutokea na kuharibu mipango ya siku zijazo ya nchi. Kwa hali hii KANU itaelekeza shabaha zake kwenye miradi ya kimazingira na mipango inayosimamia baraza la kitaifa la kimazingira. Umuhimu maalum utawekwa kwenye mipango ya kuzuia uchafuzi na mipango ya kiafya ya kimazingira itakayohusika na uchafuzi wa maji, hewa na ardhi.

#### **4. Utumizi wa Ardhi**

4.1. Ardhi ni maliasili muhimu ya kitaifa na serikali ya KANU inaambatanisha umuhimu mkubwa kwenye matumizi ya ardhi kwa njia ya busara.

4.2. Serikali ya KANU imesimama imara na kujitolea kikamilifu katika kupanga matumizi ya ardhi kwa njia za uhifadhi wa kimazingira, kwa upimaji wa ardhi, usaraveya pamoja na kuwapatia makazi wananchi wa Kenya ili kuhakikisha maslahi ya kiuchumi na kijamii kwa manufaa ya wananchi.

4.3. Kufuatana na haya, Serikali ya KANU inaongeza juhudi ili kurahisisha utolewaji wa hati za kumiliki ardhi ili wananchi wa Kenya wapate nafasi ya kupata mikopo kwa ajili ya usitawi wa kilimo na kibiashara. Kwa sababu hiyo makampuni ya ununuaji wa mashamba yameamuriwa kushirikiana na serikali katika shughuli hii.

4.4. Serikali ya KANU pia imeweka umuhimu maalum ili kurudia upya sheria kadha wa kadha zinazohusika na ardhi.

4.5. Chama cha KANU kimekwisha tambua kwamba ipo haja kubwa inayokuwa ya upimaji wa ardhi ili kila mwananchi anayehusika ajipatie hati kamili ya umilikaji ardhi anayoweza kuitumia kama dhamana ya kupata mikopo ya kutumia ya kujiendeleza yeye mwenyewe kibinafsi, na kwa njia hii, juhudi zitafanywa na Serikali ya KANU kuharakisha upimaji wa ardhi ili wananchi halisi wa Kenya wapate nafasi ya kupata mikopo kwa ajili ya usitawi wa kilimo na wa kibiashara.

#### **5. Idadi ya Watu na Utumizi wake**

5.1. Kukua kwa haraka kwa idadi kubwa ya watu nchini kunatokana na kuongezeka kwa uzazi na upungufu wa vifo. Kwa kutegemea kiwango hiki cha kukua tunaweza kuwa na idadi ya watu milioni 24.9 katika mwaka 1990, na milioni 37.5 katika mwaka 2000. Hali hii inayoongezeka inatarajia kuondolewa kwa

muda fulani. Kwa hivyo juhudi za Serikali ya KANU zitaelekezwa kuimarisha ubora wa maisha na kuhudumia idadi kubwa ya watu watakao kuwepo pamoja na hawa waliopo kwa hivi sasa. Nguvu za wananchi wetu zitategemea masilahi ya jumla ya idadi ya watu nchini.

5.2. Serikali ya KANU inatambua haja ya kuendeleza masilahi ya hali ya juu ya wananchi pamoja na kazi wanazoweza kufanya watu na kuzithamini kama rasilmali muhimu ya kimsingi nchini mwetu. Ni kwa sababu hii Serikali ya KANU itaelekeza kwa umuhimu mkubwa zaidi ili kusitawisha maliasili ya binadamu kama msingi wa kuendeleza maendeleo kwa jumla. KANU itafanya kila juhudi ili iimarisha ujuzi kwa wananchi kwa kupatikana mazingira yanayohitajika na mazingira yanayomtia hima kila mwenye bidii na ili kuongeza uzalishaji wa kila mtu binafsi. Katika juhudi zake za kuimarisha masilahi na uzalishaji kwa wananchi wetu, Serikali ya KANU itahakikisha kwamba mahitaji ya kimsingi na huduma yanapatikana na wananchi wote. Ni lazima isisitizwe kwamba kupatikana kwa haja za kimsingi ni sharti ya kwanza muhimu kwa ajili ya kupatikana kwa maendeleo ya jumla ya kiuchumi na ya kijamii. Kwa kuzingatia maslahi ya wananchi, Serikali ya KANU itahakikisha kwamba hizi haja na huduma za kimsingi zilizokwisha tajwa zinapatikana kwa jamii.

5.3. *Afya.*—Maendeleo makubwa kabisa yamekwisha patikana tangu uhuru kwa ajili ya kuimarisha afya ya wananchi. Kiwango cha kufa watu ovyo, kufa kwa watoto wachanga kumepungua sana na wakati huo huo kupatikana kwa maisha kwa wakati wa uzazi kumeimarika barabara. Huku kupungua sana kwa wakati wa vifo na kupatika kwa maisha marefu kwa wananchi kunaonyesha dhahiri jinsi afya ilivyokuwa imeimarika nchini. KANU imeidhamiria kuendeleza hali hii kwa kupatikana kwa huduma za afya na mfumo mkamilifu wa afya kama vile ujenzi wa wadi za Nyayo kwenye mahospitali mengi nchini.

5.4. *Chakula na Lishe.*—Kupatikana kwa maisha mazuri kwa wananchi kunatokana na aina ya chakula bora kinacho thibitisha hali ya lishe kwa wananchi wetu. Uchunguzi wa hivi karibuni unaonyesha kwamba kwenye kipindi cha muda fulani, kwenye kiwango cha kitaifa, kumekuwa na maendeleo, ingawa ni madogo, katika hali ya lishe. KANU itaendelea kufanya juhudi na kuhimiza mipango yenye lengo la kuimarisha hali ya lishe ili kurahisisha matumizi bora ya maliasili ya binadamu.

5.5. Chakula ni mahitaji ya msingi kwa ajili ya masilahi ya wananchi. Serikali ya KANU imesimama imara na kujitolea kikamilifu ili kuhakikisha kwamba nchi inaweza kujitegemea katika uzalishaji wa chakula. Serikali ya KANU itafanya juhudi kuhakikisha kupatikana kwa usalama wa chakula nchini na hasa kwenye maeneo yasiyopata mvua ya kutosha na kwenye maeneo makavu, maeneo ambayo hukumbwa na ukame mara kwa mara. Utafiti unaowezekana utatumiwa na kuhimizwa kwenye sekta ya kilimo ili kuongeza mapato ya mazao shambani kwa kila hekta ya ardhi inayolimwa. KANU inakusudia kupanua juhudi za kuhimiza uzalishaji wa mazao ya vyakula na mazao yanayouzwa nje kwa kutumia usimamizi unaofaa na kutumia barabara mali zote zinazoingizwa kwenye kilimo.

5.6. *Maji.*—Serikali ya KANU itaendelea na juhudi zake thabiti za kupatikana kwa maji masafi kwenye kila nyumba. Ili kufanikisha juhudi hizi nafasi ya jamii kwa njia za harambee pamoja na kuyalipia maji yatakuwa ni mambo ya umuhimu mkubwa sana.

5.7. Serikali ya KANU itaendelea kupanua mipango iliyopo hivi sasa ya kujenga visima vya maji, mabwawa, misingi ya maji pamoja na mitaro ili maji yapatikane kwa matumizi ya binadamu na ya mifugo kwenye maeneo yasiopata mvua ya kutosha na kwenye maeneo makavu nchini.

5.8. Mamlaka ya Bonde la Ziwa, Mamlaka ya Mto wa Tana na Mto wa Athi na Mamlaka ya Bonde la Kerio, zote zitapanua mipango yake ili maji yanayopatikana kutoka kwenye maziwa na mito itumike kwenye shughuli za umwagiliaji maji, matumizi ya nyumbani na kwa ajili ya kustawisha nishati na stima inayopatikana kwa kutokana na nguvu za maji.

5.9. *Mpango wa Jamii wa Majira.*—KANU itapanua juhudi zake za kuendeleza mipango ya uzazi wa majira kama jambo muhimu la kwanza kitaifa kwa lengo la kupunguza idadi ya kukuwa ya wananchi kila mwaka ya kiwango cha asilimia 4.1 na kuhakikisha kwamba wananchi wanayo, na wanapata, idadi ya watoto wanaoweza kuwalea na kuwasimamia kikamilifu na bila ya kuwa na matatizo yasiyo ya kawaida. Ili kupatikane lengo hili Serikali ya KANU inafikiria kuweko kwa familia ya kiasi ambayo itakwenda sambamba na rasilimali ya kiuchumi ya taifa pamoja na matarajio ya wananchi wake.

5.10. *Elimu*.—Serikali ya KANU inatambua kwamba elimu ni moja ya mambo yanayoweza kuathiri sana ubora wa maisha. Elimu ndiyo inayojenga msingi wa ufundi unaoweza kuendeleza na kuboresha hali ya maisha. Pia kuweza kuathiri ubora wa afya na hali ya nyumba na ni kwa kutokana na haya ndipo Serikali ya KANU ikawa inasisitiza juu ya mpango wa nidhamu katika elimu. Kwa hivi sasa Serikali ya KANU imekwisha tekeleza mpango wa elimu wa miaka 8-4-4 ambao utakuwa ukitumika kikamilifu ufikapo mwaka wa 1990 kuanzia shule za msingi na kuendelea hadi vyuo vikuu.

5.11. Ikiwa na lengo la kutoa ujuzi wa kufanya kazi kwa wote, mpango wa elimu wa 8-4-4 utatoa mchango wake wa kupunguza kiwango cha kutopatikana kazi kwa wanafunzi wanaotoka mashuleni. Serikali ya KANU itaendelea kuwa thabiti na kujitolea ili kuboresha elimu ya manufaa kwa watoto wote wanaokwenda mashule. Pamoja na elimu ya ufundi, na mafunzo ya kufanya kazi, Serikali ya KANU itahakikisha mafunzo ya viwango vya juu ya kufanya kazi yanapatikana kwenye vyuo vyote vya ufundi nchini.

5.12. Kupatikana kwa nyumba mbali kuwa ni mahitaji ya kimsingi kupatikana kwa nyumba, kunaathiri afya na lisehe ya wananchi ni kidokezo muhimu cha kiwango cha maisha. Serikali ya KANU itakusudia kulipa umuhimu wa kwanza swala hili la kupatikana kwa nyumba kwa jumla na hasa kupatikana kwa nyumba sehemu za mashambani. Serikali ya KANU itajitahidi kupatikana kwa nyumba zikiwa na mahitaji muhimu kama vila maji, vituo vya afya na mashule yaliyo karibu karibu.

5.13. *Huduma kwa Jamii*.—Katika juhudi za kustawisha maeneo ya mashambani, Serikali ya KANU ikishirikiana na jamii zinazoishi mashambani pamoja ha mashirika mengine, itafanya juhudi kupatikana kwa mahitaji kadha wa kadha. Serikali ya KANU itakuwa na lengo la kupatikana kwa urahisi mahitaji kadha wa kadha kama vile mashule, vituo vya afya, masoko na barabara za mashambani ili ziwe karibu na mahali wanakoishi wananchi.

5.14. *Usitawi wa Vijana*.—Mfumo wa wananchi wetu kimsingi ni wa vijana, kwani asilimia hamsini (50%) ya idadi ya wananchi ina umri wa chini ya miaka kumi na mitano. Kwa hivyo kundi hili la wananchi linahitaji kupewa umuhimu mkubwa. Pia kundi hili

lina matatizo makubwa ya kutegemea wananchi wengine. Serikali ya KANU kwa hivyo itaelekeza rasilimali kubwa ili iweze kuwaendeleza vijana wa nchi hii wapate kuwa raia waaminifu wa kuzalisha mali. Misaada itapelekwa kwenye vyuo vya ufundi vya mashambani na juhudi zitafanywa na serikali ya KANU kutoa mafunzo bora zaidi ya kikazi ili walemavu, yaani wasiojiweza, waweze kushiriki kikamilifu na kujiingiza katika shughuli za kijamii.

5.15. *Wanawake katika Maendeleo.*—Serikali ya KANU inatambua shughuli za wanawake zinazoendelea kama uti wa mgongo wa uchumi wa kitaifa, na hasa katika uzalishaji wa kilimo. Jambo la fahari zaidi ni la wanawake kuweza kujitayarisha na kuunda vikundi vya kujisaidia wenyewe vya akina mama. Lengo la KANU ni kuvigeuza vikundi hivi viwe ni vikundi vya maendeleo na kukua kwa taifa.

5.16. Serikali ya KANU itaendelea kuunga mkono elimu ya wasichana kwenye viwango vyote na kujihusisha kwa wanawake katika nyanja zote za maendeleo ya kiuchumi nchini. KANU itaendelea kutambua na kuendeleza nafasi kwa wanawake katika huduma zinazotolewa katika Serikali na kwenye sekta nyingine za uchumi.

## **6. Utafutaji wa Nafasi za Kazi**

6.1. Kupatikana kwa kazi maana yake ni kuzishughulisha na kuzitumia rasilimali zinazotokana na binadamu kwenye maeneo ambako yatakuwa na manufaa kabisa kiuchumi. Wasiwasi wa Serikali ya KANU, kama unavyokaririwa kwenye Waraka wa Kikao nambari mbili wa mwaka 1985, si kuanzisha sekta mpya ya kusababisha kupatikana kazi, lakini lengo hasa ni kurahisisha uzalishaji wa kila mojawapo wa watu katika kundi la wafanyi kazi.

6.2. Kukosekana kwa kazi kwenye mazingara yetu maana yake ni kutopatikana kwa nafasi za kupata mapato kutokana na kazi au kutokana na kazi za binafsi. Kwa hivyo ni lengo la Serikali ya KANU kuwepo nafasi zaidi za kazi kwa wale wanaotafuta kazi hivi sasa, na kuongeza uzalishaji wao. Kwa hivi sasa wafanyi kazi wanaoweza kufanya kazi nchini Kenya wanakadiriwa kuwa asilimia themanini na tano (85%) ya idadi yote ya watu wafanyao kazi. Asilimia kumi na tano (15%) iliyobaki ni ya watu

wasiojiweza au wasioweza kufanya kazi kwa sababu kadha wa kadha. Kwa kutokana na kiwango kikubwa cha uwezo wa kufanya kazi, Serikali ya KANU imekusudia kutumia njia zote zinazowezezana ili kupunguza tatizo la ukosefu wa kazi.

6.3. Serikali ya KANU inatambua kwamba sababu kubwa za ukosefu wa kazi nchini ni pamoja na kiwango kikubwa cha kukua kwa idadi ya watu, na kwa hivyo kuongeza idadi ya wale wanaotafuta kazi: kutoweza kwa uchumi kukua kwa kiwango ambapo kingeweza kusababisha kazi nyingi zaidi za kuwaajiri wale wote wanaotafuta kazi: kukosekana kwa mizania ya ujuzi: ufundi usiofaa na matatizo ya ucheleweshaji wa kutekelezwa kwa miradi kwenye mipango mikubwa ya maendeleo. Serikali ya KANU kwa hivyo itafuata sera na mipango itakayoweza kupanua sekta zote za makampuni na ya Serikali kwenye uchumi ili zipate kusabasisha kupatikana kwa kazi.

6.4. Serikali ya KANU inaamini kwamba tatizo la kupata kazi ni lazima lishughulikiwe kwa msingi wa muda mrefu. Sera za muda mrefu zitakazotumiwa ni pamoja na kubana matumizi ya fedha ili kusababisha nafasi zaidi za kazi, kutoa vihimizo vitakavyotia moyo uzalishaji wa rasilimali na uhusiano wa kimataifa unaofaa ili kudumisha masoko ya nje. Serikali ya KANU itahakikisha kwamba sera hizi zinatumika na kutekelezwa. Na zaidi Serikali ya KANU itajitahidi kutekeleza hatua za muda mfupi kupunguza matatizo ya wakosao kazi. Hizi ni pamoja na kupunguza ukubwa wa familia, marekebisho ya mfumo wa elimu kubadili nadharia na matarajio ya kazi, kuimarisha usimamizi wa afya, nyumba bora, na kupatikana kwa mahitaji ya kimsingi ambayo yataongeza uzalishaji wa wafanyi kazi.

6.5. Katika jaribio la kusababisha nafasi za kazi, Serikali ya KANU itasisitiza kupatikana kwa kazi kwenye sekta hizi.

6.5.1. *Sekta ya Kisasa.*—Tangu uhuru Sekta ya Kisasa imesajili kukua kwa haraka. Maendeleo haya katika sekta hii hayakugeuzwa kwa kusababisha kazi zaidi ili kuwaajiri wale wanaotafuta kazi wanaozidi. Serikali ya KANU inakusudia kuelekeza juhudi za dhati ili kuifanya sekta hii itoe kazi nyingi zaidi kwa kutumia ufundi unaofaa.

6.5.2. *Sekta ya Viwanda.*—Serikali ya KANU itahakikisha kwamba sera yake kuhusu viwanda ina lengo la kutoa kazi kwa

wingi. Kazi hii ni lazima itekelezwe kwa gharama ndogo na kuhakikisha maendeleo yanayofaa kwa viwanda wakati ambapo sehemu kubwa ya kutoa kazi itapatikana kwenye sekta nyingine. Serikali ya KANU inataraji kwamba viwango vya sasa vitapanua uwezekano wa kupatikana kazi kwa haraka zaidi kuliko sekta nyingine kwa rasilimali mpya, matumizi ya uzalishaji ya rasilimali na mipango mipya itakayolinda rasilimali na wakati huo huo kutumia wafanyi kazi zaidi.

Serikali ya KANU itahakikisha kwamba sekta ya kutengeneza bidhaa imejengwa juu ya uwezekano wa uzalishaji mkubwa na utakaoweza kuwavutia wafanyi biashara wadogo wadogo na mameneja wa wananchi halisi wa Kenya. Kukua kwa viwanda ni lazima pia kuunge mkono na kupanua maendeleo ya kilimo na ya sehemu za mashambani.

6.5.3. *Sekta ya Kilimo.*—Inatambuliwa na Serikali ya KANU kwamba sekta ya kilimo itaendelea kuongoza nchi katika maendeleo ya kiuchumi. Serikali ya KANU inakusudia kusisitiza umuhimu wa uzalishaji mkubwa kwenye sekta ya kilimo, na kulinganisha jambo hili pamoja na sera nyingine ili ziwe zinaathiri mapato yanayozidi kwa wananchi wanaokaa mashambani. Kuongezeka kwa uzalishaji kutakua ni chanzo muhimu cha kukua. Serikali ya KANU imeona ya kwamba kupatikana kwa kazi kwenye hekta moja kunawezekana zaidi katika mashamba madogo kuliko mashamba makubwa. Mashamba madogo pia yameonyesha uzalishaji mkubwa zaidi. Serikali ya KANU kwa hivyo itawahimiza wazalishaji kwenye mashamba madogo.

6.5.4. *Sekta Isiokuwa ya Serikali.*—Serikali ya KANU inaelewa kwamba shughuli kwenye sekta isiyokuwa ya Serikali nchini imekabiliwa na matatizo kadha yanayoweza kutatuliwa kwa kuzirekebisha sera yake na kwa kuipa msaada moja kwa moja ili kupanua uzalishaji, na kwa kufanya hivyo kwa kuongeza upatikanaji wa kazi.

6.5.5. Ili kupunguza matatizo ya sekta hii, Serikali ya KANU inakusudia kutumia vyuo kama vile vya ufundi kwa vijana ili kuanzisha ufundi bora zaidi kwenye sekta hii. Serikali ya KANU itaihusisha sekta hii kikamilifu na vyuo vya ufundi kwa vijana. Serikali ya KANU pia itaendeleza matumizi ya bidhaa na huduma zinazotolewa na sekta hii.

6.5.6. Shida kubwa ya maendeleo kwenye sekta isiyokuwa ya Serikali ni ukosefu wa fedha za kutosha. Serikali ya KANU inakusudia kuanzisha mfumo mzuri utakaoweza kutoa mikopo kwenye sekta hii. Na ili kuongoza uzalishaji kwenye sekta hii, Serikali ya KANU inakusudia kupanga usimamizi ulio rahisi wa mipango ya mafunzo kwa mafundi walio wadogo wadogo kwenye nyanja mbalimbali. Uwezekano wa sekta hii wa kutoa kazi kwa vijana ni lazima kusesitizwe. Wengi wa wafanyi kazi wa sekta hii wamo katika lile kundi la idadi ya watu nchini wenye umri wa kati ya miaka kumi na mitano (15) na ishirini na minne (24). Kwa hivyo kukosekana kwa kazi kwa vijana kunaweza kupunguzwa sana kwa kutoa misaada kwenye sekta hii.

## **7. Mpango wa Uwekaji Rasilimali**

7.1. Serikali ya KANU imekuwa na wasiwasi kuhusika na uzalishaji mdogo wa rasilimali nchini. Waraka wa Kikao Nambari Moja wa 1986 unaonyesha kwamba sababu moja ya kupungua kwa uzalishaji wa rasilimali upo katika mfumo wa bei za bidhaa muhimu, zikilinganishwa na zile bidhaa zinazoongeza bei ya rasilimali inayotakikana kwa ajili ya kuzalisha mali. Ili kupambana na tatizo hili Serikali ya KANU itaanzisha vivutio zaidi ili viweze kuweka rasilimali kwenye shughuli zisizohitaji rasilimali kubwa kubwa.

7.2. Katika miaka kumi iliyopita rasilimali ziliwekwa kwenye vikwazo vilivyolindwa na kutekelezwa miradi ya rasilimali kwa gharama kubwa. Serikali ya KANU itafanya juhudi kupunguza vikwazo hivi vilivyolindwa na itatumia vivutio vya masoko kupanua rasilimali kwenye maeneo ya uzalishaji. Serikali ya KANU itarekebisha upya sera za biashara ili kupunguza kiwango cha kulinda na hasa kwenye shughuli za kuzalisha bidhaa zitakazo tengenezwa humu humu nchini, kuendeleza viwango vifaavyo vya riba, na kupanua shughuli ndogo ndogo za kutungeneza bidhaa na za huduma.

7.3. Ili kuhakikisha kuongezeka kwa rasilimali serikali ya KANU itahakikisha kwamba sera za rasilimali zipo wazi na zenye mipango. Itarudia upya na kutekeleza kwa mpango sheria ya uhifadhi wa rasilimali za kigeni. Ili kuwatia moyo wawekaji akiba wa kigeni wapate kuzileta rasilimali zao humu nchini.

7.4. Serikali ya KANU pia itahakikisha kwamba ushirikishwaji kikamilifu wa Wakenya unapatikana kwa kuwahusisha na kuukabidhi uchumi kwa wananchi halisi wa Kenya. Kwa hivyo KANU italeta mazingira ya kuukabidhi uchumi kwenye mikono ya wananchi halisi bila ya kuwavunja moyo wawekaji rasilimali kutoka nje, ambao haki zao zimelindwa na sheria ya Bunge.

7.5. Ili kuhakikisha upanuzi wa masoko kwa ajili ya bidhaa zetu za viwandani, serikali ya KANU itatimiza ushiriki kikamilifu kwenye biashara ya kimataifa kuanzia kwa nchi za jirani. Juhudi mahasusi zitafanywa kutega biashara katika maeneo ya biashara nafuu, yaani P.T.A. Serikali ya KANU pia itahakikisha ya kwamba bidhaa zinazotengenezwa viwandani mwetu ni vya hali ya juu na bei zake zinalingana vyema na bei za kimataifa.

7.6. Kupatikana kwa stima mashambani kutaharakishwa ili kuvutia kuwekwa kwa rasilimali mashambani na kwa ajili ya kuhimiza viwanda vidogo vidogo. Ni lengo la serikali ya KANU kuimarisha rasilimali zinasopatikana nchini kwa kupitia juhudi za mipango za kamati ya maendeleo ya wilaya ili kuongeza shughuli za viwanda mashambani.

7.7. *Utafiti na Maendeleo.*—Serikali ya KANU imetambua manufaa ya utafiti, sayansi na ufundi ili kupatikane usitawi unaotakikana. Wizara mpya iliyoundwa imeiweka Kenya kati ya yale mataifa yenye mfumo wa kikweli kwa ajili kutathmini, kupanga na kusimamia maendeleo. KANU itazidi kuziendeleza juhudi hizi.

7.8. Kuhusika na rasilimali katika mashirika ya Serikali, sera ya serikali ya KANU, kila itakapowezekana itabaki kuwa mashirika haya ni lazima yalete faida. Kwa hivyo mashirika ya Serikali, makampuni, na kadhalika yatakuwa yakirudiwa mara kwa mara ili zipangiwe hatua za kufuata.

## **8. Ulinzi na Usalama wa Ndani.**

8.1. Serikali ya KANU inaamini kwamba usalama unaunga mkono maendeleo. Kama vile maendeleo yanavyounga mkono usalama.

8.2. Serikali ya KANU itaendeleza kuwepo na kurahisisha kuwepo kwa jeshi ambalo litalinda na kuhakikisha usalama wa ndani na heshima ya mipaka yetu.

8.3. Kwa hivyo Jeshi la Kenya, Jeshi la Wanamaji la Kenya, na Jeshi la '82 la kikosi cha wanaahewa vyote vitakuwa katika hali imara na kupewa vifaa vya kulinda Kenya dhidi ya uchokozi wowote kutoka nje.

8.4. Kikosi cha Polisi cha Kenya na Kikosi cha Polisi cha Utawala vyote pamoja vitaendelea kudhibiti na kuimarisha shughuli zao za usalama, kwa kuhakisha kwamba sheria za Kenya zinatekelezwa, na wakati huo huo hatua zinachukuliwa kuboresha sura yao kwa wananchi.

8.5. Wananchi wataendelea kuhimizwa kuunga mkono vyombo vya kulinda usalama wa ndani katika kuendeleza amani na utulivu kwenye sehemu za mashambani na kwenye viwango vya vijiji.

8.6. KANU kama chombo cha wananchi wote kitafanya juhudi kuvunjilia mbali vikwazo vya kiukoo na vya kikabila vinavyozorotesha kuwepo nadharia ya taifa moja na fahari ya kitaifa ya kibinafsi na kuwa ni tisho kwa usalama kwa kitaifa.

8.7. Serikali ya KANU kama matokeo ya Katiba ya Kenya inaunga mkono muundo mzima uliomo humo. Na hasa chama kitaendelea kuimarisha na kulinda haki na uhuru wa kimsingi wa kila Mkenya binafsi pamoja na wengineo lakini wakati huo huo chama kitahakikisha kwamba haki za wengineo haziingiliwi ovyo na mtu yeyote.

8.8. *Kazi ya Vijana wa KANU.*—Vijana wa KANU watahimiwa kutoa mchango wao katika kulinda maisha na mali huko vijijini na kwenye maeneo yaliyo jirani wakishirikiana kikamilifu na utawala wa mikoa na polisi ya Kenya.

8.9. *Faini ya Kufanyishwa Kazi.*—Serikali ya KANU itaimarisha kutekelezwa kwa kuwafanyisha kazi wale wahalifu wanaovunja sheria ndogo ndogo.

8.10. *Uhusiano wa Wafanyi Kazi.*—Serikali ya KANU itahakikisha kwamba Wanakenya wanaendeleza haki yao ya kuwa wanachama wa shirika la COTU pamoja na vyama vingine vinavyohusiana na COTU. Ni jambo la furaha kwa KANU kwamba vyama vya wafanyikazi vinalinda masilahi yao, huboresha uzalishaji na amani kwenye viwanda. KANU siku zote itaunga mkono na kuzilinda juhudi hizi.

## 9. Siasa ya Nje

9.1. Msingi wa pamoja wa siasa ya nje ya Kenya ulijengwa wakati wa kuunda chama cha Kenya African National Union (KANU) katika miaka ya kwanza ya 1960. Kuanzia wakati wa uhuru, Jamhuri hii changa imekuwa imara na kujitolea kikamilifu kufuata siasa ya nje ikiongozwa na misingi ifuatayo:

- (a) Ujirani Mwema.
- (b) Ushirikiano wa Kimajimbo.
- (c) Ukombozi Kamili wa Bara la Afrika.
- (d) Siasa ya Kutofungamana na Upande Wowote.
- (e) Amani na Usalama wa Kimataifa.
- (f) Ushirikiano wa Kiuchumi wa Kimataifa.

9.2. *Ujirani Mwema.*—KANU inaamini kwa dhati juu ya siasa ya ujirani mwema na ya kudumisha utulivu wa kimajimbo. Kwa hivyo serikali ya KANU haitakuwa na dhamira mbaya kwa yeyote lakini itaendelea kama ilivyofanya hapo zamani kunyosha mkono wa urafiki kwa nchi zote. Jambo la kwanza na muhimu ni kuunda na kuhakikisha mazingira mazuri ya kuishi pamoja na amani yatakayoleta maendeleo ya haraka katika jimbo lote. Siasa ya KANU ya nje juu ya ujirani mwema umebakia haujabadilika.

9.3. *Ushirikiano wa Kimajimbo.*—KANU imefanya juhudi kupanua na kurahisisha ushirikiano wa kimajimbo kwenye daraja zote. Njia hii iliyofuata siasa ya kufana imeendelezwa na kuzihusisha pia nchi zilizo mbali na jirani zetu kama inavyoonekana katika kujihusisha kwetu kikamilifu katika shughuli mbali mbali za kimajimbo kama vile eneo la biashara nafuu, mamlaka inayohusu serikali kadha juu ya ukame na kupanuka kwa jangwa, na mpango wa uchukuzi wa mlango wa kaskazini.

9.4. Kwa kutokana na maendeleo ya haraka, afya iliyoimarishwa, elimu, na mambo mengineyo, manufaa ya ushirikiano wa kimajimbo yamekuwa na maana zaidi. Kutokana na haya, Serikali ya KANU imepanua juhudi zake katika ushirikiano wa kimajimbo.

9.5. KANU inaamini kwamba ushirikiano kama huu utakuwa ni wa manufaa kwa pande zote zinazohusika.

9.6. *Ukombozi Kamili wa Bara la Afrika.*—KANU imejitolea ili kupatikane uhuru kamili wa Bara la Afrika. Haya ni mapambano yanayohusu heshima ya Waafrika na heshima ya utu


wa binadamu wote. Kwenye kiwango cha kimataifa, Serikali ya KANU itaendelea kutoa misaada ya hali na mali kwa vyama vya ukombozi vya Afrika Kusini na Namibia.

9.7. *Siasa ya Kutofungamana na Upande Wowote.*—Siasa ya KANU ya kutofungamana na upande wowote imejengwa juu ya misimamo ya usawa kati ya mataifa, kuishi kwa amani kwa pamoja, kuheshimiana na kutoingilia mambo ya ndani ya mataifa mengine. Kenya inataka urafiki na kila taifa litakalofanya vivyo hivyo. Kenya imesimama imara na kujitolea kikamilifu kwa kuunga mkono yale inayoamini kuwa ni sawa na ya haki katika masuala ya kimataifa.

9.8. *Amani na Usalama wa Kimataifa.*—Kwa kuwa KANU inaheshimu na kupenda ubinadamu kumetufanya sisi kusimama imara na kujitolea ili kuendeleza usalama na amani ya kimataifa na utatuzi wa kiamani juu ya mizozo. Kwa hali hii tunaamini kwamba kuendeleza kwa amani na usalama, kukiwepo kwa nia njema ya wote kutaweza kupatikana kwa viwango vya chini vya silaha na kuwaongoza katika hali ya jumla ya kuondoa silaha zote.

9.9. *Ushirikiano wa Kimataifa.*—KANU inaamini kwamba ili kupatikane kukua kiuchumi kiulimwengu kutaweza kupatikana katika mazingira ya heshima na ya kufanyiana usawa. Kwa hivyo tutaendelea kuunga mkono na kufuata juhudi zenye lengo la kuleta mfumo mpya wa kimataifa wa kibiashara na wakifedha.

9.10. Ikiwa inatambua siasa hizi za kitaifa, chama kitaendelea kupanua ushirikiano wa kimataifa unaohitajika ili taifa letu lipate maendeleo. Chama kwa hivyo kitaendelea kunyosha mkono wa kirafiki kwenye nyanja za kibiashara za kifundi na za kifedha. Pamoja na jukumu la kuleta hali ya kuelewana na kuimarisha uhusiano na nchi nyingine, chama kitabeba mzigo wa kuongeza na kupanua uhusiano na harakati za kibalozi pamoja na nchi zote za ulimwengu.



**Rais Moi aongoza kuzuia mmomonyoko wa udongo.**

**RAIS AJENGA NCHI  
KANU YAJENGA NCHI  
FUATA NYAYO!!!**

NATIONAL ASSEMBLY LIBRARY  
ACCESSION No. ....



**Wananchi wafuatā nyayo zake Rais Moi kwa vitendo!!**



**RAIS AJENGA NCHI!!**

**FUATA NYAYO!!**

## WIMBO WA TAIFA

1.

Ee Mungu nguvu yetu  
Ilete baraka kwetu.  
Haki iwe ngao na mlinzi  
Natukae na undugu  
Amani na uhuru  
Raha tupate na ustawi.

2.

Amkeni ndugu zetu  
Tufanye sote bidii  
Nasi tujitoe kwa nguvu  
Nchi yetu ya Kenya,  
Tunayoipenda  
Tuwe tayari kuilinda.

3.

Natujenge taifa letu  
Ee, ndio wajibu wetu  
Kenya istahili heshima  
Tuungane mikono  
Pamoja kazini  
Kila siku tuwe na shukrani.

## NATIONAL ANTHEM

1.


O God of all creation  
Bless this our land and nation.  
Justice be our shield and defender,  
May we dwell in unity,  
Peace and liberty;  
Plenty be found within our borders.

2.

Let one and all arise  
With hearts both strong and true.  
Service be our earnest endeavour,  
and our Homeland of Kenya,  
Heritage of splendour,  
Firm may we stand to defend.

3.

Let all with one accord  
In common bond united,  
Build this our nation together  
and the glory of Kenya  
The fruit of our labour  
Fill every heart with thanksgiving.



NATIONAL ASSEMBLY LIBRARY  
ACCESSION No. 3947  
LOCATION .....

**HAKI**

**IWE NGAO**

**NA MLINZI**